

Nipashe, tarehe 12/11/2020,
Uk. 15

*Zaidi ya mbwa 500 wanaofugwa wapewa chanjo

Na Renatha Msungu,
DODOMA

HALMASHAURI ya Jiji la Dodoma imetoa chanjo ya mifugo kwa mbwa 502, wanaofugwa majumbani ili kubabiliana na magonjwa mbalimbali hususani tatizo la kichaa cha mbwa.

Mkuu wa Idara ya Mifugo na Uvuvi wa Halmashauri ya Jiji la Dodoma, Gration Mwesiga, alibainisha hayo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu operesheni ya utoaji chanjo kwa wanyama inayotekelizwa na wataalamu wa mifugo.

Mwesiga, alisema lengo ni ku-

wafikia mbwa wote wanaofugwa katika jamii ili kuepuka kuleta madhara kwa watu, hususani kichaa cha mbwa wanapowan-gata binadamu.

Alisema kuwa, pamoja na watu wengi kufuga mbwa, lakini hawawapeleki katika chanjo, jambo ambalo halikubaliki kitalamu.

"Tumejipanga kuhakikisha tunatoa chanjo kwa mbwa wote hapa jijini, tunahitaji kuona mbwa wanaofugwa wanakuwa katika hali ya usalama ili wasilete matatizo kwa jamii," alisema Mwesiga.

Alisitiza jamii kuhakikisha wanapeleka mifugo yao, kupa-ta chanjo pale wanaposikia

kuna utoaji huduma hiyo, zoezi linalotekelizwa na watalaamu wa mifugo, katika maeneo yao.

Alisema, hakuna sababu ya wao kufuga mifugo, bila kufuata taratibu za kiafya kwa wanyama ambayo inawasaidia kuwa katika hali ya usalama.

Pia, alisema bado wataende-
lea na operesheni ya kuua mbwa
wanaozurura mitaani ili kuepu-
sha kuleta madhara ya kichaa
cha mbwa.

Alisema kumekuwa na tabia
ya jamii kusuga mbwa na ku-
waachia wakizurura oyo kitendo
kisichokubalika na idara ya
mifugo inaendelea na operesh-
eni hiyo.

"Bado tunaendelea na zoezi

la kuua mbwa wazururaji lengo
ni kuepusha kuwasababishia
binadamu kichaa cha mbwa,"
alisema Mwesiga.

Aidha, alisema operesheni
hiyo imefanyika katika mitaa
mbalimbali jijini Dodoma na ku-
dai kuwa wataendelea kuwas-
ka mbwa hao na kuwatokomeza
kabisa.

Aliwataka wananchi kutoa
taarifa wanapoona kuna mbwa
wanazurura ili wasiendelee ku-
leta madhara.

Kitaalamu alisema, mbwa
mzururaji hupata kichaa, ku-
tokana na kukosa matunzo au
kuumwa na wanyama wengine
kama ipaka na fisi ambaa hum-
sababishia kichaa.